



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



TAARIFA KWA UMMA

**UTEKELEZAJI WA AGIZO LA SERIKALI - BAADHI YA MABASI YA MASAFI
MAREFU KUANZA SAFARI SAA 11:00 ALFAJIRI**

Tarehe 16 Disemba, 2022, Mhe. Jumanne A. Sagini (Mb), Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitoa ridhaa kwa baadhi ya mabasi ya masafa marefu kuanza safari saa 11.00 alfajiri. Utekelezaji wa ridhaa hiyo uliambatana na masharti mbalimbali likiwemo sharti la madereva wa magari yatakayopewa ratiba hizo kuwa wamethibitishwa na kusajiliwa na Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413 ili kurahisisha ufuatiliaji wa madereva na udhibiti wa ajali zinazosababishwa na makosa ya kibinadamu. Ridhaa hii ya Serikali ilipokelewa vizuri na wamiliki pamoja na madereva wa mabasi ya masafa marefu.

Katika kikao cha pamoja cha kutathmini utekelezaji wa ridhaa hii kati ya LATRA, Jeshi la Polisi-Kikosi cha Usalama Barabarani na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA) kilichofanyika Ofisi za LATRA Mkoa wa Dar Es Salaam, Ijumaa, tarehe 13 Januari, 2023, wasafirishaji waliomba Mamlaka kushauriana na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani ili kuangalia upya baadhi ya masharti ya kupata ratiba za kuanza safari saa 11:00 alfajiri na kurahisisha upatikanaji wake. Mamlaka ilizingatia maombi ya TABOA na kufanya mashauriano ya Kamati Maalum ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani katika kikao kilichofanyika tarehe 14 Januari, 2023, Dar es Salaam.

Hivyo, Mamlaka inapenda kuutaarifu Umma kwamba, LATRA imeridhia maombi ya TABOA na kwamba watoa huduma wanaohitaji ratiba ya kuanza safari saa 11:00 alfajiri wanatakiwa kuwaelekeza madereva wao kuwasilisha maombi ya kusajiliwa kwenye ofisi za LATRA zilizo karibu nao. Hatua za uthibitishaji wa madereva hao zitafuata baada ya kupatiwa ratiba husika wakati huduma zikiendelea kutolewa. Maombi ya usajili yatumwe kwa njia ya kieletroniki kupitia anwani <https://rrims.latra.go.tz/>. Aidha, Mamlaka imefungua kituo cha usajili wa madereva kwenye Ofisi ya LATRA iliyopo Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam ambacho kitakuwa kinatoa huduma kila siku kuanzia saa 11:00 alfajiri hadi saa 4:00 usiku.

Maombi ya kusajiliwa yaambatishwe na nyaraka zifuatazo:-

- (i) Leseni ya udereva;
- (ii) Namba ya Kitambulisho cha Taifa (NIDA);
- (iii) Cheti cha taaluma ya udereva kutoka Chuo kinachotambulika na Serikali; na
- (iv) Taarifa ya Uthibitisho wa afya kutoka Hosptali ya Serikali. Fomu inayomuwezesha dereva kuomba uthibitisho wa afya inapatikana kwenye tovuti www.latra.go.tz na ofisi za LATRA.

Kwa maelezo zaidi piga simu bila malipo 0800110019.

Imetolewa na:
Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano – LATRA
15 Januari, 2023